BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Saba – Tarehe 18 Mei, 2023**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):**

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu Hotuba ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora (Bajeti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali) kwa Mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

131. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Zanzibar bado haina nguvu kazi yenye utaalamu wa kutosha kuuhudumia utalii wenye tija kwa raia na kwa Serikali, hali inayolazimisha kuwategemea raia wengi wa kigeni kuutumikia na kunufaika na huduma za kitalii za Zanzibar. Hata hivyo, bado hakuna matayarisho yanayoridhisha kuelekea utegemezi wa Wazanzibari kwenye sekta ya utalii katika visiwa vya Zanzibar.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani katika kuandaa na kuzisimamia taasisi za kutoa mafunzo na kuwajengea uwezo wa kiushindani vijana wetu, ili waweze kuajirika katika ngazi zote muhimu katika sekta ya utalii.

(b) Je, ni upi utaratibu rasmi wa sasa ambao unahakikisha mfumo wa majukumu ya mashirika au wawekezaji kwa jamii (Corporate Social Responsibility) unasimamiwa na kufanya kazi kwa maslahi ya jamii husika.

(c) Je, ni kwa kiasi gani Serikali inahakikisha kipaumbele cha ajira kinakuwa kwa wazawa kuanzia ngazi za juu hadi za chini kulingana na sifa na uwezo wao (merit and competency) wa utekelezaji wa ajira hizo.

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

23. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Naipongeza Serikali kwa mradi mkubwa wa ujenzi wa soko la Machomane katika jimbo la Wawi.

(a) Je, ujenzi huo utagharimu kiasi gani cha fedha.

(b) Je, ni lini ujenzi huo utakamilika rasmi na soko kuanza kutumika.

<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>

92. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Mfumo wa sasa wa kuwepo kwa Benki Kuu (BoT) ambayo, pamoja na mambo mengine, inasimamia sera za kifedha na sarafu haujaisaidia sana Zanzibar katika kukuza uchumi wake kwa kasi inayostahiki.

(a) Je, ni ipi tathmini ya kitaalamu ya karibuni ya mfumo wa fedha na mabenki ulioangalia ukuaji bora wa uchumi wa Zanzibar.

(b) Je, ni kwa vipi mfumo wa sasa unatoa fursa kwa kila upande wa Muungano kusimamia sera zake za kifedha bila ya kuingiliwa.

(c) Je, Serikali haioni ulazima kwa kila upande wa Muungano kuwa na benki ya eneo husika (State Bank of Zanzibar & State Bank of Tanzania) ambazo zitasimamia sera za kifedha na kuiwacha Benki Kuu (BoT) kubaki kama msimamizi wa sarafu ya Tanzania pekee.

<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>

66. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Tumeshuhudia duniani kote jinsi mchezo wa riadha unavyofuatiliwa na kupendwa nchi mbali mbali zinachukuwa juhudi kubwa ya kuushughulikia mchezo huu ikiwa ni pamoja na kuwatayarisha wana riadha tokea wakiwa wanafunzi katika skuli zao mbali mbali.

(a) Je, ni lini Wizara yako itaushughulikia mchezo wa riadha kama inavyoushughulikia mpira wa miguu hapa nchini.

(b) Mchezo wa riadha kwa hivi sasa, ndio mchezo unaoweza kutuletea heshima kimataifa. Je ni lini Wizara yako itawaleta makocha wanaoijua riadha ili kuwafundisha wana riadha wetu.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

33. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa kumekuwa na mfumko mkubwa wa kuanzishwa kwa vyuo katika ngazi ya cheti na diploma hapa Zanzibar.

(a) Je, Serikali inaonaje kuanzisha mtaala mmoja utakaotumika kufundishia vyuo hivyo kulingana na programu husika inayotolewa katika chuo husika.

(b) Je, vyuo hivyo vinasimamiwa na nani.

(c) Kwa kuwa kila chuo kina mtaala wake na utaalamu ama wataalamu wake, je ni kwa kiasi gani tunaweza kupima ubora wa elimu inayotolewa katika vyuo hivyo.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

12. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika miezi ya hivi karibuni kumekuwa na manung’uniko mengi ya wananchi katika baadhi ya maeneo ya Unguja na Pemba kwamba, mfumo wa maji safi umekuwa na harufu mbaya katika maji yanayotumika majumbani pamoja na majengo ya ibada, jambo ambalo ni hatari kwa afya zao.

(a) Je, kwa kiasi gani Serikali inalitambua jambo hili.

(b) Je, ni hatua gani zinachukuliwa kudhibiti jambo hili.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

35. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

(a) Je, Serikali kupitia Wizara ya Afya inasimamia vipi uendeshaji wa programu za afya zinazotolewa katika vyuo binafsi “private”.

(b) Kwa kuwa muhitimu aliyesoma “private” anaweza kuajiriwa na Serikali, Je, ni chombo gani kinachosimamia ubora na ufanisi wa programu za mafunzo katika vyuo hivyo, ili kupata madaktari bora ambao wanaenda kushughulika na uhai wa watu.

36. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa kumekuwa na mkataba wa Serikali kupitia Wizara ya Afya na Kampuni ya kuagiza dawa na kusambaza katika Bohari zetu.

(a) Je, kuna mashirikiano gani kati ya kampuni na wataalamu (Watibabu) katika hospitali zetu.

(b) Je, ni kiasi gani cha uingizaji wa dawa unaoendana na uhitaji au mapendekezo ya wataalamu ambao wapo hospitali.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

68. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika Bajeti ya mwaka 2022/2023, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipanga kuzifanyia matengenezo barabara zilizojengwa kwa lami laini kisiwani Pemba zikiwemo barabara ya Mtambile – Mwambe, Mtambile – Kangani, Mizingani – Wambaa – Kenya – Chambani na nyenginezo, lakini mpaka sasa barabara hizo bado hazijajengwa.

(a) Je, Mhe. Waziri kuna sababu gani mpaka sasa zilizopelekea kutokujengwa kwa barabara hizo.

(b) Je, Wizara yako ina mpango gani mwengine wa kuzijenga barabara hizo.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

126. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Pamoja na jitihada za Serikali za kushajiisha vyanzo vyengine vya kuuendesha uchumi na utambulisho wa Zanzibar, bado zao la karafuu na biashara ya utalii vinaonekana kuwa na nafasi kubwa katika uchumi wa Zanzibar. Hata hivyo, msimu uliopita ulikumbwa na kero nyingi kwa wananchi kutoridhishwa na mwenendo wa Serikali wa kutowajali wananchi wala maoni yao juu ya njia bora ya kulishughulikia zao la karafuu.

(a) Je, ni ipi tathimini ya Serikali juu ya jamii kutoridhishwa na mwenendo wa Serikali wa kutoyashughulikia malalamiko na maoni yao juu ya njia bora ya kulishughulikia zao la karafuu.

(b) Je, ni yepi marekebisho yaliyofanyika ili kuondoa kero zilizojitokeza katika kulishughulikia zao la karafuu kwa ufanisi.

(c) Je, Serikali imefikia wapi katika utaratibu wa kuibinafsisha biashara ya karafuu kwa wananchi na kuweka utaratibu maalum wa utambulisho wa karafuu kutoka Zanzibar katika soko la kimataifa.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

57. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kumekuwa na tabia ya kuwatesa sana wanyama kwa kuwatuma kupita kiasi na kuwapiga sana.

(a) Je, Serikali inaumia vipi kuona wanyama wanatumwa na kuteswa nchini.

(b) Je, ni hatua gani kama Wizara mlizozichukua katika kulikomesha suala hili.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka 2023/2024.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka 2023/2024.

Zanzibar,
18 Mei, 2023.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA